## Our Vision

"A credible electoral management body committed to strengthening democracy in Kenya."

## Our Mission

"To conduct free and fair elections and to institutionalize a sustainable electoral process."

## Our Core Values

- Integrity
- Team work
- Independence Innovativeness
- Respect

## 1.0 Utangulizi

Uchaguzi mkuu wa mwaka huu utafanyika mnamo siku ya **Jumanne** tarehe **nane mwezi wa Agosti** katika maeneo yote ya uwakilishi bungeni kote nchini. Shughuli hii pia itafanyika katika mataifa ya Uganda (Kampala), Tanzania (Dar es salaam na Arusha), Burundi (Bujumbura), Rwanda (Kigali) na nchi ya Afrika Kusini (Pretoria).

## 2.0 Je, ni akina nani watapiga kura tarehe nane Agosti 2017.

Wapigakura wote waliomo kwenye Rejesta ya wapigakura watapiga kura siku hiyo. Kila mmoja wao anahitajika awe:

(i) Na kitambulisho halisi au paspoti halali ya Kenya aliyotumia kujiandikisha kuwa mpigaji kura.

(ii) Amejitokeza yeye mwenyewe katika kituo cha kupiga kura.

## 3.0 Je Uchaguzi utafanyika wapi?

**Upigajikura tarehe 8 Agosti utafanyika katika:**

(i) vituo vyote vya kupigia kura katika wodi zote elfu moja, mia nne na hamsini.

(ii) Afisi za ubalozi wa Kenya zilizoko katika nchi za Uganda (Kampala), Tanzania (Dar es saalam na Arusha), Rwanda (Kigali), Burundi (Bujumbura) na nchi ya Afrika Kusini (Pretoria).

(iii) Magereza nchini Kenya ambayo yametengwa kirasmi kuwa vituo vya kupiga kura.

## 4.0 Ni wakati gani ambapo upigaji kura utaanza na kumalizika?

(i) Upigaji kura utaanza **saa kumi na mbili asubuhi** na kumalizika saa **kumi na moja jioni** kote nchini Kenya na nchi za ngambo husika .

(ii) Wapiga kura wote wataokuwa kituoni kufikia saa kumi na moja wataruhusiwa kupiga kura.

(iii) Iwapo kituo cha upigaji kura, kitachelewa kufunguliwa saa kumi na mbili asubuhi kwa sababu moja au nyingine, muda wa kupiga kura katika kituo hicho utaongezwa.

## 5.0 Ni viti gani ambavyo mpigakura atapigia kura?

a) Mpigakura atampigia kura kiongozi anayemtaka kukalia viti vifuatavyo:

(i) Rais

(ii) Mbunge/Mjumbe

(iii Mwakilishi wa Wodi

(iv) Seneta

(v) Mwakilishi wa Wanawake katika bunge

(vi) Gavana

b) Mpigakura mkenya atakayepigia kura nchi za Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi au Afrika Kusini atampigia kura mgombeaji anayemtaka wa **Uraisi pekee yake.**

## 6.0 Je, Mpigakura atafanya nini akifika kituoni?

Pale kituoni, Mpigakura anahitajika:

(i) kutoa kitambulisho halisi au paspoti halali kwa karani wa IEBC

(ii) kuwekelea kidole kwa mashine ya KIEMS ili aweze kutambukiwa kwa njia ya eletriniki.

(iii) kupokea makaratasi sita ya kupigia kura yaliyopigwa muhuri wa IEBC,


(iv) kuelekea katika eneo la kupigia kura kwa siri.

(v) kutia alama sahihi katika makaratasi yote **sita** ya kupigiakura.

(vi) kutumbukiza kila karatasi la kura kwenye sanduku ambalo kifuniko chake ni rangi sawa na karatasi la kupigiakura.

(vii) Kupakwa wino isiyofutika kwenye Kidole kuthibitisha kuwa tayari amepiga kura.

(viii) kuondoka kituoni baada ya kupiga kura.




*Utaratibu wa kupiga kura*

## 7.0 Mpigakura atafanya nini iwapo hana uwezo wa kusoma wala kuandika?

**Mpigakura wa aina hii:**

(i) Atachagua mtu wa miaka 18 na zaidi anayemiliki kitambulisho au Paspoti ya Kenya amsaidie kupiga kura

(ii) Mtu anayesaidia mpigakura huyo awe Msaidizi anahitajika kuchukua na kutia sahii fomu ya kiapo cha kuweka siri ya kura

(iii) Afisa wa IEBC anayesimamia kituo atamsaidia mpigakura wa aina hii asiyekuwa na msaidizi lakini mbele ya maagenti wa vyama.

## 8.0 Mpigakura atafanya nini iwapo hajatambuliwa kieletroniki na mashine ya KIEMS?

Mpigakura ambaye hajatambuliwa kieletroniki na mashine ya KIEMS anahitajika kujaza Fomu 32A ili kuruhusu atambuliwe kwa kutumia nambari ya kitambulisho chake au Paspoti.

## 9.0 Ni teknolojia gani itakayotumika siku ya kupiga kura?

Mnamo siku ya uchaguzi, Tume itatumia teknolojia inayoitwa KIEMS, yaani Kenya Integreted Elections Management System. Kila kituo cha kupigia kura kitakuwa na mashine ya KIEMS itayokuwa imewekwa Rejesta ya Wapigakura wa kituo hicho.

Mashine hizi zitatumika:

(i) Kutambua wapigakura kwa njia ya elektroniki.

(ii) Kupeperusha matokeo ya uchaguzi kwa njia ya kielektroniki.



*Picha ya mashine ya KIEMS*

## 10.0 Je, ni watu gani wanaoruhusiwa kwenye vituo vya kupigiakura

(i) Wapigakura
(ii) Maofisa wakuu wa IEBC
(iii) Maofisa wa kulinda usalama
(iv) Afisa wa uchaguzi anayesimamia kituo.
(v) Afisa wa uchaguzi msaidizi .
(vi) Makarani wa IEBC
(vii) Wagombeaji viti mbalimbali.
(viii) Maajenti wa vyama na wa wagombeajibinafsi.
(ix) wanahabari waliodhinishwa na IEBC
(x) Waangalizi waliodhinishwa na IEBC
(xi) Mtu mwingine yeyote anayekubalisha na Tume

## 11.0 Utaratibu wa kutangaza na kupeperusha matokeo ya uchaguzi mkuu.

Tume imeteua vituo vitengo vitatu vya kuhesabia, kutangazia na kupeperushia matokeo ya uchaguzi mkuu kama ilivyoelezwa na michoro hii.




*Michoro inayoonyesha vituo vya kuhesabia, kutangazia, na kupeperusha matokeo ya uchaguzi mkuu*

### (i) Kituo cha kuhesabia matokeo ya uchaguzi katika eneo bunge (Constituency Tallying Centre)


Afisa anayesimamia kituo hiki ni Afisa msimazi wa Uchaguzi Katika Eneobunge (Constituency Returning officer).

Afisa huyu anahesabu matokeo ya uchaguzi yanayotoka kwenye vituo vya kupigia kura katika eneo lake na kutangaza mshindi wa kiti cha;

a) Mbunge wako


b) Mwakilishi wa Wodi

## Polling Station
## Electronic Presidential Result Transmission
## (FORM34 A)





## FOMU RASMI ZA KUTANGAZA MATOKEO YA MBUNGE NA MWAKILISHI WA WODI

### (Declaration and Certification of Winner's at the Constituency level)




WINNER
NATIONAL
ASSEMBLY





WINNER
COUNTY
ASSEMBLY

### (ii) Kituo cha kuhesabia matokeo ya uchaguzi katika Kaunti ( County Tallying Centre)

Afisa anayesimamia kituo hiki ni Afisa wa Kusimamia uchaguzi katika Kaunti. Katika kiwango hiki Afisi msimamizi wa uchaguzi katika Kaunti hupokea matokeo ya maeneo bunge, huhesabu, hujumulisha na kutangaza mshindi wa kiti cha;

- (i) Senata
- (ii) Mwanamke Mwakilishi wa kaunti katika bunge
- (iii) Gavana


## FOMU RASMI ZA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI WA SENATOR,MWAKILISHI MWANAMKE KWA BUNGE LA KITAIFA NA GAVANA



### (iii) Kituo cha Kitaifa cha kuhesabia matokeo ya uchaguzi wa Urais ( National Tallying Centre)

Afisa anayesimamia kituo hiki ni msimazi wa uchaguzi wa Urais, ambaye ni Mwenyekiti wa IEBC. Mwenyekiti wa IEBC hupokea, kuhesabu, kujumulisha na kutangaza matokeo ya uchaguzi wa urais.

**FOMU RASMI ZA KUJUMULISHA MATOKEO YA UCHAGUZI WA URAIS**





**FOMU RASMI YA KUTANGAZA MSHINDI WA UCHAGUZI WA URAIS**




**WINNER**
**PRESIDENTIAL ELECTION**

## IEBC KUWEKA WAZI MATOKEO YA UCHAGUZI WA URAIS




### 12.0 kuishi kwa amani na utangamano kabda, wakati wa na baada ya uchaguzi mkuu

Tume huru ya uchaguzi na mipaka, IEBC inahimiza wananchi wote kuishi kwa amani na utangamano kabla, wakati wa na baada uchaguzi

**Kura Yako. Maisha Yako!**

**TUME HURU YA UCHAGUZI NA MIPAKA**

Anniversary Towers, 6th Floor, University way

P.O Box 45371-00100, Nairobi Kenya.